MISINGI YA IMANI #2

Katika somo la Misingi ya Imani #1 tuliona:

1. Kwamba dhambi iliingia ulimwenguni na Mungu amesema “Wote wametenda dhambi.”
2. Kwamba mshahara wa dhambi ni mauti.
3. Kwamba karama ya Mungu ni uzima wa milele.
4. Kwamba tunatakiwa “Kumfuata Kristo” kama Paulo aliye mtume wa Matifa alivyomfuata.
5. Kwamba sisi tulio Kanisa lililo Mwili wa Kristo tuna kazi ya huduma ya upatanisho (2 Wakorintho 5:18-20).

Ili mwanafunzi aelewe “ufunuo wa siri” uliofunuliwa kwa mtume Paulo katika kitabu cha Waefeso, ni lazima mwanafunzi huyu atambue kwamba Mungu hubadilisha mahusiano yake na watu katika madaraka (vipindi vya mipango ya Mungu ndani ya historia) tofauti; ingawa kanuni za Mungu hazibadiliki. (Utajifunza zaidi kuhusu Teolojia ya Madaraka katika somo lifuatalo linaloitwa “Kuielewa Biblia.” Kwa sasa inatosha kujua kwamba madaraka yanahusu masharti na mipango ya Mungu kwa ajili ya watu wake na wanadamu wote katika vipindi maalum vya historia.)

Ukisoma Mathayo 10:5,6 na Waefeso 3:8,9 utaona mfano wa badiliko moja lililotokwa kati ya madaraka mawili. Ukisoma Marko 12:31 na Wagalatia 5:14 utaona mfano wa kanuni ya Mungu ambayo haibadiliki wakati madaraka yamebadilika.

Kanisa lililo Mwili wa Kristo, lilianzishwa na huduma ya Paulo aliye mtume wa watu wa Mataifa (1 Wakorintho 3:5-11). Kanisa hili halikutajwa na waandishi wengine wa Neno la Mungu (Waefeso 3:1-8). Paulo alianza huduma zake mara baada ya kuokolewa katika barabara ya Dameski, muda fulani baada ya Pentekoste (Matendo 9).

Wakati unaendelea na masomo haya zidi kumwomba Mungu amfanye Roho Mtakatifu kukusaidia na kukufundisha kwa sababu ukweli wa neno la Mungu hauwezi kueleweka kikamilifu bila msaada wa Roho Mtakatifu kukupa ufahamu .

SEHEMU YA KWANZA

MAAGIZO MAKUU MATATU

1. Wengi wanadhani “Agizo Kuu” la Mathayo 28:19-20, ambayo ni mafundisho ya mwisho ya Yesu kwa wanafunzi wake, kuwa ndiyo agizo letu leo. Kuna matakwa au masharti gani katika agizo hilo?

   a. _____

   b. _____

   c. _____

ZINGATIA: Kadiri unavyojifunza Biblia utagundua kwamba mitume 12 walipewa agizo hili na lilikuwa mwendelezo wa huduma ambazo walikuwa wamepewa tayari. Ujumbe waliohubiri ni kuwaambia Waisraeli (au Wayahudi) kutubu ili Mungu amrudishe Kristo kuanzisha ufalme wake duniani (Matendo 1:6; 3:19-21). Ufalme huo ni ufalme wa kweli (sio wa kiroho tu) wa hapa duniani ambao uliahidiwa kwa Waisraeli katika Agano la Kale na vitabu vya Injili.

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

2. Agizo la kwanza lililotolewa na Bwana kwa wanafunzi wake na linapatikana katika Mathayo 10:5-6. Yesu aliwaambia mitume hawa 12 kutowaendea watu gani? _____

   _____

   Walitakiwa kwenda kwa watu gani? _____

3. (Mathayo 10:7-8) Walitakiwa kutangaza ujumbe gani? _____

   Walipaswa kufanya huduma zipi?_____

   _____

4. Je, Mungu anataka tulifuate agizo hili leo? _____ Ndiyo _____ Hapana

5. (1 Wakorintho 1:22; Yohana 6:28-30) Katika agizo hili Bwana Yesu aliwapa wanafunzi wake uwezo wa kuponya, kutakasa ukoma, kufufua wafu n.k. Kwa nini? _____

   _____

   Ishara hizo zililenga Wayahudi au Mataifa?_____

6. (Matendo 28:28) Baada ya Mungu kuacha kujishughulisha na taifa la Israeli, Injili ilitumwa kwa watu gani?

   _____

7. (Warumi 11:11) Wakati Israeli (taifa la Wayahudi) walipokataa thawabu ya Mungu ya kupewa ufalme, kwa nini Mungu alianza kuwageukia mataifa?_____

8. Mungu alipoacha kulishughulikia taifa la Israeli (kwa muda) kama taifa lake maalum la agano na kuwageukia mataifa, agizo la Mathayo 28:19-20 liliwekwa pembeni. Mtume Paulo alipewa agizo jipya kwa ajili ya Kanisa lililo Mwili wa Kristo. Tafadhali soma 2 Wakorintho 5:18-20. Mstari wa 18 unasema tumepewa nini?

   _____

9. (2 Wakorintho 5:18-19) Huduma tuliyo nayo leo ni "Huduma ya upatanisho" ambayo inalenga watu wote ikiwa ni pamoja na Wayahudi na Mataifa. Huduma yenyewe ni kwa hawa watu kuokolewa kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Sisi Wakristo wa leo tunaitwa nani katika mstari wa 20?_____

10. (Wagalatia 1:8) Kutatokea nini ikiwa mtu atahubiri Injili nyingine tofauti na ile ambayo Paulo alihubiri?

    _____

11. (Warumi 1:16; Matendo 13:46) Katika kipindi cha mabadiliko ndani ya kitabu cha Matendo, kipau mbele katika kuhubiri Injili kilifuata mpangilio gani (watu gani kwanza)?_____

    _____

12. (Matendo 28:28) Upendeleo huu wa kuhubiria Wayahudi kwanza uliisha katika Matendo 28. Kuanzia muda huo *"Wokovu huu wa Mungu umepelekwa kwa"* nani?_____

13. (Warumi 11:25) Ni wakati gani ambao Mungu ataanza kujishughulisha na taifa la Israeli tena kama watu wake maalum?_____

14. (Warumi 11:26-27) Mungu ataleta ukombozi na wokovu kwa ajili ya Israeli kama taifa tena lini?_____

    _____

15. Je, leo Wayahudi wanaweza kuwa wajumbe wa Kanisa lililo Mwili wa Kristo?_____

    Waefeso 2:16 inasemaje? (Tumia maneno yako mwenyewe) _____

    _____

    _____

    _____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

16. (Waefeso 2:19) Katika Kanisa lililo Mwili wa Kristo kundi gani la watu limepewa upendeleo? Zungushia moja:
    Wayahudi Mataifa Hakuna
17. (Waefeso 2:12) Watu wa Mataifa walikuwa na hali au nafasi gani kabla ya kuanzishwa kwa Kanisa lililo Mwili wa Kristo?
    a. _____
    b. _____
    c. _____
    d. _____
    e. _____
18. (Waefeso 2:14) Mungu amebadilishaje hali hii ya Mataifa? _____
    _____
19. Soma Wakolosai 3:11 na Wagalatia 3:28. Je kuna kundi lolote katika Mwili wa Kristo ambalo laweza kupokea heshima maalum au nafasi maalum kuliko makundi mengine? Ndiyo _____ Hapana _____.
    Kwa nini? (Angalia sehemu za mwisho za mistari hii) _____

KUTIMIZA AGIZO LETU

20. (1 Wakorintho 4:1) Jukumu na baraka za waumini walio katika Mwili wa Kristo ni nini?_____
    _____
21. (Warumi 12:2) Tunawezaje *"Kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu"*?
    _____

Ili mtu ajue mipango ya Mungu kwa ajili yake kila siku lazima awe na bidii katika kusoma Neno la Mungu. Pia anatakiwa kuwa na uwezo wa kutofautisha kati ya migawo ya Neno la Mungu ili ajue ni maagizo gani yanayomlenga na yasiyomlenga.

23. Tafadhali soma: Wafilipi 3:17; 4:9; 2 Timotheo 2:2; 2:7; 1 Wakorintho 11:1; 1 Wakorintho 14:37. Paulo anatusihi kufanya nini katika mistari hii?_____
    _____
24. (1 Wakorintho 15:1-4) Mwili wa Kristo umepewa Injili ya Kristo. Injili ya Kristo ni nini?_____
    _____
25. (1 Wathesolanike 2:4) Tunenavyo?_____
    _____
26. (2 Timotheo 2:2) Tutatimizaje agizo tulilopewa katika Kanisa la leo?_____
    _____
27. (Tito 2:13) Tumaini la Kanisa lililo Mwili wa Kristo ni nini?_____
    _____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

SEHEMU YA PILI

Katika sehemu ya kwanza tuliona:

a. Kuwa "ndani ya Yesu" leo ni kuwa ndani ya Kanisa lililo Mwili wa Kristo.
b. Kwamba hakuna mwandishi mwingine yeyote ndani ya Biblia aliyelitaja Kanisa lililo Mwili wa Kristo isipokuwa Paulo tu.

Katika somo hili fupi haiwezekani kuchimba sana ndani ya mafundisho haya. Tungependa kusisitiza tena hitaji lako la kumwomba Mungu wakati unajifunza Neno lake ili akusaidie kuelewa vizuri zaidi. Kama somo hili la msingi litakuwashia hamu ya kujifunza Biblia zaidi, basi litakuwa limefanya kazi yake.

Kama Waberoya uchunguze Neno la Mungu lenye thamani kubwa lakini uwe mwangalifu ukisikiliza onyo la 2 Timotheo 2:1,2: *"Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu. Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."*

1. (Waefeso 1:20-23; 5:23) Katika barua za Paulo (na siyo sehemu nyingine yoyote ya Biblia) tunaona neno "Kanisa" linamaanisha "Mwili wa Kristo." Nani ni kichwa cha Mwili huu?_____
2. (Wagalatia 1:1,12) Mtume Paulo alipokeaje Injili aliyoihubiri?_____
   _____
3. (1 Wakorintho 12:13) Mtu hupata kuwa mjumbe wa Kanisa namna gani?_____
   _____
4. Katika 1 Wakorintho 12:14 Paulo anasema, *"Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi."* Je wewe ni kiungo cha Mwili wa Kristo? Ndiyo _____ Hapana _____
5. Je una uhakika kwamba wewe ni mjumbe wa Mwili wa Kristo? Jibu kwa kutumia maneno yako mwenyewe. (Majibu yatatofautiana)_____
   _____
6. (Warumi 10:13) Je, mtu yeyote anaweza kuwa kiungo cha Kanisa, Mwili wa Kristo?_____
   _____
   (Wagalatia 3:26) Kuna sharti gani ili mtu awe mjumbe wa Kanisa lililo Mwili wa Kristo?_____
   _____

MSTARI WA KUKARIRI - 1 WAKORINTHO 12:27
"Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake."

7. (Waefeso 3:8) Mtume Paulo alipewa neema (baraka) gani kama mhubiri maalum kwa ajili ya Kanisa?
   _____
8. (Waefeso 3:9) Paulo alikuwa na jukumu gani?_____
   _____
9. Soma Warumi 16:25-26 na Waefeso 3:1-6. Tunajifunza nini kuhusu ufunuo wa siri katika Warumi 16:25 na Waefeso 3:5? _____
   _____
10. (1 Wakorintho 2:13) Nani ni mwalimu wetu tunapotafuta kuelewa mambo ya Mungu?_____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

11. (Wakolosai 1:9-10). Tunahitaji hekima na ufahamu kutoka kwa Mungu ili tuweze kutumia ukweli wa Neno la Mungu katika maisha yetu kila siku. Kweli_____ au Si kweli _____
12. (Wakolosai 2:6-7) Paulo anataka waumini waishije?
    a. _____
    b. _____
    c. _____
    d. _____
13. Biblia inatoa onyo gani katika Wakolosai 2:4?_____
    Katika Wakolosai 2:8?_____
    _____
14. (Waefeso 1:15-19) Taja mambo matano aliyoyaomba Paulo kwa ajili ya waumini wa Efeso?
    a. _____
    b. _____
    c. _____
    d. _____
    e. _____
15. (Waefeso 6:11-13) Biblia inatupatia maelekezo yapi ili tuweze kusimama dhidi ya hila za shetani?_____
    _____
16. Kwa mujibu wa Waefeso 6:12, Tunashindana na nini?_____
    _____
    _____
17. (Waefeso 6: 14-17) Orodhesha silaha 6 za silaha za Mungu.
    a. _____
    b. _____
    c. _____
    d. _____
    e. _____
    f. _____
18. Kwa mujibu wa Waefeso 6:18:
    a. Tunatakiwa kuomba wakati gani?_____
    b. Tunatakiwa kuombaje?_____
    c. Tuombe kwa ajili ya nini?_____
19. (Waefeso 6:19-20) Paulo anawaomba Waefeso kumwomba Mungu nini kwa ajili ya Paulo mwenyewe?_____
    _____

<u>1 WATHESOLANIKE 5:16-18</u>

FURAHINI SIKU ZOTE
OMBENI BILA KUKOMA
SHUKURUNI KWA KILA JAMBO
MAANA HAYO NI MAPENZI YA MUNGU KWENU KATIKA KRISTO YESU

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

MAMBO MATATU YA KUAPA

1. UAMUZI WA KUJITOA KWA MUNGU – Warumi 12:1-2

   Kuishi kwa Kristo kunaanza na uamuzi wa kujitoa 100% kwake. Ni uamuzi wa kila siku. Tena ni uamuzi unaoonekana katika matendo yenyewe ya kujitoa kwake. Kama Mkristo, unapaswa kutii Warumi 12:1-2 na kujitoa hali na mali kama sadaka kwa ajili ya mambo ya Mungu. Je, umewahi kufanya uamuzi wa kujitoa kwa Mungu? Je, unaendelea kufanya uamuzi huo?

2. UAMUZI WA KUTOJITOA KWA DHAMBI - Warumi 6:11-13

   Kuishi kwa Mungu ni kutoishi kwa dhambi, ni kujiwazia kuwa mfu kwa dhambi. Yaani mfu hawezi kutenda wala kujaribiwa na dhambi hivyo Mkristo anapaswa kujihesabu kuwa mfu kwa dhambi ili asitii dhambi na kujihesabu kuwa hai kwa Mungu ili amtii Mungu. Wakristo sio watumwa tena kwa dhambi (6:6) na hivyo wanaweza kuamua kuitii au kutoitii. Uamuzi unaotakiwa ni ule wa kutotii dhambi. Je, unajihesabuje? Umefanya uamuzi wa kutojitoa kwa dhambi? Je, unarudia uamuzi huo kila siku?

3. UAMUZI WA KUMRUHUSU MUNGU KUFANYA KAZI NDANI YAKO - Wagalatia 2:20

   Yesu na Roho Mtakatifu wanakaa ndani yetu sisi tulio waumini. Kusudi la kukaa ndani yetu ni kutujenga na kutubadilisha kufanana naye (Wafilipi 1:6). Vilevile ni kutufanya tuishi kwa ajili yake Yesu na siyo kwa ajili yetu. Ndiyo maana anasema *"wala si mimi tena."* Roho Mtakatifu anatuwezesha kujitoa kwa Mungu na anatuwezesha kutojitoa kwa dhambi tukimruhusu. Wakati Roho Mtakatifu anatuongoza ndani ya mioyo yetu tunapaswa kuamua kumtii, kumfuata, na kutembea naye. Je, unamruhusu Roho Mtakatifu kuongoza maisha yako?

"KRISTO ANAISHI NDANI YANGU"

Hali hii ni kweli wa kila muumini.

"KRISTO ANAISHI KUNIPITIA MIMI"

Hali hii siyo kweli kwa kila muumini. Ni kweli tu kwa wale wanaomruhusu Yesu kuishi kuwapitia, yaani wale wanaokubali kutawaliwa naye ili maisha yao yatimize mapenzi ya Yesu

Tumia nafasi hii kuandika maswali au maoni yoyote uliyo nayo:

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Rudisha somo hili kwa:

_____ Namba yetu ya simu_____

_____

_____

Habari zako:

Tarehe: _____ Jina lako:_____

Anwani yako: _____

Mji: _____Namba yako ya Simu:_____

_____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship